Tuzungumze

Eti wandumba wa Bukavu washambulia Kivu ya Kaskazini !

Mpanda ovyo hula ovyo a mpenda yote akosa yo- e. Maneno hayo ya mu- gwana hayakosi maana ama habari toka Goma, ji mkuu wa Wilaya ya ivu ya Kaskazini ni ya weli. Sikieni tena ma- bo mengine ya wandumba a Bukavu.

Msomaji wetu Shabani- wayanga Kap. ajiuliza ama maisha ya dada wa- ojawamoja wa leo yata- ikilia hali gani siku ijazo. Kwani akitoa ano wa mji wa Goma ye- nasi twasikitika na venendo wa dada hao.

Ingawa mji wa Goma ni ango wa kuingilia ji- oni mwa Kivu toka anja wa ndege na mipaka nchi jirani kazaa, tu wengi huwaza kama i wa Goma umegeuka stani wa anasa ambako weza kushimika mitego zaa ili kufikilia aīs maisha mazuri.

Bila uwongo, mji huo Goma wawavuta watu ngi, wananchi kama vi- wageni juu ya uzuri ke na mambo kazaa ya alii. Lakini siku hizi gonjwa wa "kipindu- ndu" waushambulia. onjwa huo si ungine li mashambulio ya dada tu toka mjini Bukavu. hawa hushambulia mji Goma kama nzige za- mbulia mimea shamba- . Kweli mzee mungwana a haki ya kusema : utamkuta msichana (ki- na mke, binti) anaye- zarau".

Siku kwa siku, tuki- ungua vema maisha ya sichana hao yatele- ana. Kwani huwaona, ada ya kusifia ujinga o, huzururazurura mi- ani kama mabata yasi- kuwa uwani wala yasi- we na mwenyeji wakido- adowea kama nzi kwenyi ungi wa pombe. Na bila ga hutia pua popote ofisini (biro) na pe- inepo wakitafuta lwa ombe ao sabuni" kama a wenyi kutangatanga sijue wakwendako. Na ko washikwa mateka na kari-jeshi wahusikao uchunguzi, utafuti na alama mjini ama BSRS. ni wengi kati ya dada hawana vikartasi vya mbulisho (C.I. na ka- ika). Ni wahuni ao?

Zaidi ya hayo, asema msomaji wetu Shabani, dada zetu malaya, hao, hawana nafasi ya kujipumzisha iwe usiku wala mchana. Ni hivi kutokana na magumu hayo, huanza kuwauzi wavulana (vijana wanaume) wajani (célibataires) ao wasio bado na wanawake wawapatie mahali ya kupiga usingizi. Pia waliweza kuvumbu uwerevu ungine. Uwerevu huo ni wakusikilizana wamalaya watano ao sita (5 ao 6) na kuchukua chumba kimoja kunako hoteli fulani na mwisho wa mwezi kukusanya feza za kulipa chumba hicho. Kwa kweli ukitaka kuwa na uhakikisho, wakati unapita mjini Goma, kajielekeze kwenyi mahoteli kama vile "Quel Type, Soki-Toto, Aspro, Macho-kwa-macho". Na huko utawakuta wasichana wa mtindo huo wenyi umri wa miaka 16 hadi 18 wakizungukazunguka mahoteli kama nyuki huzunguka mizinga ya asali.

Alaala ! Hum ! Siyo mji wa Goma tu. Ukaendelea safari yako zaidi kwa zaidi kaskazani mwa jimbo, utakuta miji ya Ishasha, Kanyabayonga, Butembo, Beni hata Bunia (Zaīre ya Juu) yameshambuliwa kabisa na watoro hao. Na hawa wasahau kuwa kadiri mungwana hufyonza pombe nayo humfyonza akili.

Ingawa dada zetu hao hawapendi kuishi tena pembeni ya wazazi wao, hawajifikiri kama haraka haraka haina baraka na heri twaa kama inshallah utapata. Na wakati washauriwa huko wanapoenda kuhangaika kama wa- Mahangaiko wao hujibia kama hawezi "kuuwa mwili" na eti "kya mutu cha musauver (kuponya)", eti "mpaka na mimi niuze shati la kike "makambo ezali bourreau" lile la "Mamou". Na dada hao hawatambue kama ni uharibifu wa maisha yao. Bila kusahau kuwa kuku hula kadiri ya mdomo wake na mwisho wa njia ni nyumbani.

Alamsiki

Bisimwa L.-B. Tserou.

Je umesikia...?

KUWA mungwana husema : aliyemnyima mwenzake nyama ya senji (rongeur), mbuluku akamnyima nyama ya mbogo. Masemi hayo ni ya kweli na yatokana na hali ya wakaaji wa mkoa mdogo wa Mulengeza waliomo kwa sasa. Kwani ingawa waliombwa kuachia kanisa la kiprotestanti CEPZA makao na shamba zao, leo hii wapinga hatua hilo. Kwa nini ?

Kwa kuwa kanisa hilo halikutimiza ahadi lake la kuwajengea jamaa hao nyumba 52 kama walivyoahidiwa. Sasa wajiunga mkono na wakataa kabisa kuhama kwa kuwa ni nyumba 16 tu walipewa !

Baada ya kula nyama yenyi kugonjwa watu watatu wafariki dunia

Habari toka mtaa wa Masisi, wilayani Kivu ya Kaskazini, zajulisha kuwa watu watatu walifariki dunia katika mkoa wa Gatoyi baada ya kula nyama isiyopimwa na mganga. Habari hizo zilikamilishwa na mwaandishi wetu kina dada Bujiriri Mwangaza ambaye alikuwa mapumzikoni katika wilaya hiyo.

Waliposikia habari hizo, wakuu wa serikali wilayani walimuomba mganga-kiongozi wa hospitali ya Masisi, mwananchi Mugisho, ajielekeze haraka mkoani huko ambako watu yapata 254 waliangamizwa na ugonjwa mkali wa kuhara na kutapika.

Uchunguzi na mapimo kazaa yaliyofanyika yajulisha kweli kuwa hali hiyo yatokana na nyama isiyopimwa ambayo watu watatu hao walikula. Na wengine waliopatikana na kuangamizwa vikali walikula nyama hiyo bila kuipika vizuri kulingana na kanuni za afia.

Hali hiyo haingetukia kama wakaaji waliarifiwa ama kupewa maelimisho kazaa juu ya afia. Chumba chenyi kuhusika na afia chapashwa kufan vyote kiwezavyo na ka zake vema kabisa za k waelezea wakaaji mam kazaa wa kazaa kuhu afia na kuwafasiria um himu wa kupimisha nya kwa mganga mbele ya ku uzisha, kuinunua a kuipika na baadae kuil

Basi kumbe mbele kununua, kuuzisha, kup ka nyama yafaa kuipim sha kwa mganga mwen kuhusika na kazi hi ili kuepuka hasara si za usoni. Kwani mungwan husema usipoziba u (fente) utajenga uku na uzuri wa suke (épis la muhindi waonekan ndani tu.

Bisimwa L-B. Tserou.

JUA

Gazeti la Kivu

Tarehe 27 Julay mpaka 2 Ogusti 1985

Kiongozi : Mutiri - wa - Bashara

Machache juu ya masimulizi ya Raīs Mobutu na Raia kijijini Kinkole

Mharamia Kadhafi ni mwaarabu

Kama sidanganyike, nazani kuwa, na sisi wote twajua kama Waarabu walitesa mababu utumwani na leo hii mhuni Kadhafi aliye pia Mwaarabu apoteza feza zake bure akituma watu wakukodeshwa kutia mizozo katika nchi kazaa wa kazaa ulimwenguni pahali ya kutumia feza hizo kwa kuinua maendeleo ya nchi yake ili isonge mbele. Ebu! Kitendo hicho chatezamiwa kuwa UTUMWA-MAMBOLEO (néo-esclavagisme). Na sisi twasema HATUUTAKI kwani nchi ya Zaīre ipo HURU na KUU na inayo uwezo wa kuchukua hatua ipendayo ao kufuata njia ionayo bora kwa uhusiano wake na nchi zingine. Akiendelea katika masemi yake, Raīs Mobutu alijulisha kuwa Mzaīrwa ni mtu mweusi lakini ni mtu mweusi aliye na ukoo, mbinu, mila na desturi zake za kipekee. Tulimpinga mkorofi Kadhafi nchini Tchad kwa kulinda usalama na umoja wa nchi rafiki. Leo hii kwa kuwa nchi ya Israeli iliirudishia Misri (Egypte), nchi ndugu na rafiki, vijiji na miji yake aliyoinyanganya wakati wa vita kati yao miaka iliyopita, urafiki na uhusiano kati yetu imerudishwa. Na kama safari yangu nchini huko ilimchukiza, basi kwa kumuonyesha kama tupo huru, apende asipende nitawasili mara ingine nchini Israeli siku zijazo mbele mwaka huu uishe. Na kama adai kifo cha Raīs wa Jamhuri wa Zaīre, yeye mrugaruga Kadhafi hajue kama hawezi kuwawa ? Mimi naenda vitani, natembea katika ndege, gari, mashua na vinginepo. Humo si naweza kupata kifo ? Ao yeye hawezi kuuwawa ?

Pia juu ya wana wapotevu, ilijulishwa kuwa waziri mwenyi kuhusika na uongozi wa nchi (mambo ya ndani) kuchukua hatua moja muhimu ya kuwahurumia hao wateule 13 waliotaka kuipindua serikali na wengine wananchi waliojiuzulu katika nchi za kigeni na kuipinga serikali. Ni kama vile wananchi Nguza Karl-I-bond, Mungul Diaka na wenginepo. Kwa hiyo Baba wa Taifa alinena kama hao wameisha choka na kumtusi ama kubaki mbali na nchi yao, hawa waweza kurudi nchini bila uwasiwasi wowote kwani ni watoto wa nchi Zaīre. Na watastarehe katika amani, sheria na kufanya kazi zao kama desturi sawa vile wakina Ngbenye, Soumialot, Kanza na wafuasi wengine.

Ujamii

Kulingana na maoni ya wanachama aliowaita mbele ya wakuu na wahuzuriaji ili kutoa maoni yao juu ya siasa, wanachama hao walimtolea Baba na Taifa vilio vyao juu ya usafirishaji wa wananchi, bizaa na mali zao, bei kali ya vyakula, mnyonyoko wa udongo mitaani, ununuzi wa zeluji (ciment), afia, maji na moto wa stimu kutokana na bei kali zia ndikwazo kwenyi staka bazi (factures). Kwa ma ulizo hayo, Raīs Mobut alijibu kuwa jawabu zi taweza kupatikana mnam siku zijazo na mkusary wa tarehe 24 Novemba ku nako uwanja wa tareh 20 May ndio wakati hu Raīs wa jamhuri na raī wataweza kuchungua kam matatizo yale yaliwez kupata majawabu kamili

Uhusiano

Nakuambatana na daftari ya viongozi na wakuu wa nchi rafiki na ndugu walioalikwa kusherekea nasi miaka 25 tangu nchi yetu Zaīre kupata Uhuru wake mnamo tarehe 30 Juni 1960, mfalme Baudouin na mkewe, malkia Fabiola wa Ubeleji waliwasili nchini Zaīre. Safari hiyo yalingana na uhusiano uliomo kati ya nchi hizo mbili tangu hapo Wabeleji waliohajiri (coloniser) nchi yetu na kupatia uhuru walirejea makwao. Na wakati wa safari hiyo nchini, ataonyeshwa kiasi cha maendeleo tufikiliamo kisha miaka 25 ya uhuru.

Pia katika mpango huo wa uhusiano, Baba mtakatifu wa Roma, Yoane-Paulo wa Pili, atawasili nchini Zaīre kwa mara ya pili siku za usoni. Kwa hiyo Mareshali Mobutu aliwaomba Wana-Zaīre wafanye vyote wawezavyo kwa kuwapokea waheshimiwa hao namna inavyostahili kwa kuwapokea wageni wa heshima kulingana na mila ya mababu.

BISIMWA L.-B. Tserou.